JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Telegrams: "SIASA"
Telephone: 026 2322500
Fax: 026 2323525

(Unapojibu tafadhali taja)

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi
Mtaa wa Nzuguni A
S.L.P. 2851
41220- **DODOMA**

26 Agosti 2025

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUTENGUA UTEUZI WA MGOMBEA WA URAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA - BW. WILSON ELIAS MLUUMBE NA BW. LUHAGA JOELSON MPINA**

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inapenda kuutaarifu umma kuwa, kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 4(5)(a) na (b) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, Msajili wa Vyama vya Siasa ametengua uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliokuwa wakidhaminiwa na vyama vifuatavyo:

- Alliance for Change and Transparency (ACT–Wazalendo) – Bw. Luhaga Joelson Mpina
- Alliance for Democratic Change (ADC) – Bw. Wilson Elias Mluumbe

Uamuzi huo umefikiwa baada ya Msajili kusikiliza na kupitia ushahidi uliowasilishwa na pande husika na kubaini kuwa mchakato wa uteuzi wa ndani ya vyama hivyo ulikuwa kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa (Sura ya 258), Katiba pamoja na Kanuni za vyama husika.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6A (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, chama cha siasa kinapaswa kuendeshwa kwa kuzingatia Katiba ya Nchi, Sheria ya Vyama vya Siasa, pamoja na Katiba na Kanuni zake. Hivyo, ni muhimu wagombea wakapatikana kwa njia halali na ya kidemokrasia ili kulinda utawala wa sheria, kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa.

Kwa lengo la kuimarisha uwazi na haki, vyama husika vimepewa barua rasmi za kuwajulisha kuhusu uamuzi huo wa Msajili, ambazo zimeambatishwa na maelezo ya kina ya mchakato uliotumika kushughulikia malalamiko ya wanachama wao.

Wakati huohuo, Msajili wa Vyama vya Siasa anavishukuru vyama vyote viwili kwa ushirikiano walioutoa kwa ofisi yake wakati wa kushughulikia malalamiko hayo.

Aidha, Msajili anavikumbusha vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili kuendelea kuzingatia sheria za nchi, kulinda na kudumisha misingi ya demokrasia, amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa, kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Imetolewa na;
Abuu M. Kimario
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO NA ELIMU YA URAIA**